



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO

BODI YA PAMBA TANZANIA



*Unapojibu tafadhali taja:*

Kumb. Na. TCB/ADM/VOL.XV/72

Tarehe: 26 Julai, 2022

## TANGAZO LA AJIRA YA MKATABA

Bodi ya Pamba Tanzania ni Taasisi ya Umma ambayo imeanzishwa chini ya Sheria ya Pamba Na. 2 ya mwaka 2001 na kuanza kutumika rasmi tarehe 1 Julai, 2004 kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 180 la tarehe 4 Juni, 2004.

Mkurugenzi wa Bodi ya Pamba Tanzania anawatangazia waombaji wote wenye sifa kuleta maombi ya kazi kwa nafasi ya **Mhudumu wa Ofisi** katika ofisi za Bodi ya Pamba Musoma.

### 1.0 SIFA ZA MWOMBADI

- ❖ Awe amemaliza kidato cha nne (IV) na kufaulu angalau masomo mawili yoyote.

### 2.0 MSHAHARA

- ❖ Mwombaji atakayefanikiwa, atalipwa mshahara wake kwa viwango vilivyokubaliwa na Bodi.

### 3.0 MAJUKUMU NA WAJIBU WA MHUDUMU WA OFISI

- a) Kufanya usafi wa ofisi na jengo la Bodi ya Pamba Musoma
- b) Kufanya usafi wa mazingira yanayozunguka jengo la Bodi ya Pamba Musoma.
- c) Kupokea na kuwaongoza wageni wanaofika ofisini kupatiwa huduma mbalimbali
- d) Kuandaa taarifa za malipo ya wapangaji ya kila mwezi
- e) Kutoa risiti za malipo ya wapangaji na kufuutilia ulipaji wa wapangaji hao.
- f) Utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka za ofisi
- g) Pamoja na majukumu mengine utakayopangiwa na Mwajiri.

#### **4.0 MASHARTI YA JUMLA**

- Waombaji wawe ni raia wa Tanzania wenyе umri kati ya miaka 18 na usiyozidi miaka 45.
- Waombaji wawasilishe picha 2 (passport size) za hivi karibuni.
- Waombaji waambatanishe nakala ya cheti cha kidato cha nne (IV), Cheti cha kuzaliwa na kitambulisho cha **NIDA** au namba ya NIDA ambayo ataiandika katika barua ya maombi.
- Waombaji watakaokidhi sifa zinazotakiwa ndio pekee watakaoitwa katika usaili.
- **Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 05/08/2022 saa 10:00 Alasiri katika ofisi za Bodi ya Pamba – Mwanza.**

#### **5.0 MUDA WA MKATABA**

Ajira hii itakuwa ya mwaka mmoja (1) na mkataba utakuwa ukihuishwa (**renewable**) kutegemea mahitaji na utendaji kazi.

**MUHIMU:** Kumbuka kuambatisha barua ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na nyaraka zote zinazohitajika. Maombi yote yatumwe kwa Mkurugenzi Mkuu kwa anuani ifuatayo:-

**MKURUGENZI MKUU,  
BODI YA PAMBA TANZANIA,  
S.L.P. 61,  
MWANZA.**

Barua pepe: [info@ tcb.go.tz](mailto:info@ tcb.go.tz)

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:-**

**MKURUGENZI MKUU  
BODI YA PAMBA TANZANIA**



**Jiandae Kuhesabiwa Siku ya Jumanne tarehe 23 Agosti, 2022**